**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAISI – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**


Mchinga Sekondari,

S. L. P 86,

**Lindi.**


**Ref. No……………………………..** ....…………..

Mzazi/Mlezi wa: ___________________________

S/M: _____________________________________

**YAH: KUCHAGULIWA MWANAO……………………………………………KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA YA MCHINGA KWA MWAKA WA MASOMO WA 2021.**

**1**. Jumuiya ya Mchinga Sekondari ina furaha kukujulisha kuwa kijana wako amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii ya Sekondari Mchinga kwa mwaka wa masomo 2021. Nampongeza kwa kuchaguliwa kwake.

**2**. Mtakubaliana na mimi kuwa hii ni bahati ya pekee sana kwake na muhimu sana katika kipindi cha maisha yake. Hivyo nina imani kuwa ataitumia fursa hii kwa nguvu zote, akili zote na jitihada zote. Mafanikio ya kielimu shuleni huletwa na **Nidhamu, Kujiamini, Kujituma, Kuvumilia, Usikivu, Kujielewa na Utayari/Ushirikiano wa Mzazi/Mlezi**. Mzazi tusaidiane katika kusisitiza haya, mara kwa mara!

**3**. Shule ya Sekondari ya Mchinga ni shule ya Kata ya Mchinga inayopatikana kijiji cha Mchinga II. Shule ni ya kutwa na ni mchanganyiko. Mwanafunzi atalazimika kuja shule akitokea nyumbani. Aidha, napenda kukujulisha kuwa shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** siku ya Jumatatu na hivyo mtoto wako anatakiwa kuripoti hapa shule tarehe na siku hiyo saa 1:30 asubuhi. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **......../…..../2021**. Baada ya hapo vyombo husikavya serikali vitafanya msako wa wasioripoti na kuwashughulikia kisheria.

**4**. Masomo yanayofundishwa hapa shule ni **Kingereza, Hisabati, Historia, Fizikia (Physics), Kemia (Chemistry), Jiografia, Kiswahili, Biology (Viumbe Hai), Elimu ya Dini ya Kiislamu (kwa wahitaji)** na **Literature in English (kuanzia kidato cha 3)**. Masomo yote, isipokuwa Kiswahili na Elimu ya Dini, yanafundishwa kwa lugha ya Kingereza hivyo suala la kujifunza na kukielewa Kingereza ni la muhimu sana.

**5**. Pamoja na barua hii, nimeambatanisha fomu zifuatazo ili zijazwe kikamilifu na kuwasilishwa (zile lengwa) hapa siku ya kuripoti**. Angalizo**; fomu hizi ni lazima zijazwe kikamilifu zote**.**

- Fomu Na. 1: Vipimo vya Afya (epuka kujaziwa tu, hakikisha mtoto amepimwa)
- Fomu Na. 2: Mahitaji Muhimu ya shule na Mwanafunzi,
- Fomu Na. 3: Sheria, Kanuni na Taratibu za shule,
- Fomu Na. 4: Kukiri utiifu (mwanafunzi na Mzazi/Mlezi).

Ahsante,

**KARIBUNI SANA MCHINGA SEKONDARI**

……………………………………


**SELEMANI A. MAKOPA**

**MKUU WA SHULE**

**0786 735 354**

<u>**LINDI MUNICIPAL COUNCIL**</u>

Mchinga Secondary,

P.o.Box 86,

**Lindi**.

Ref.No…………………… ………….

To the Medical Officer,

____________________,

**RE: <u>REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF ……………………………………</u>**

Please, examine the above named student and give us the report regarding his/her suitability for undertaking Secondary school studies.

1. Heart dieses ____________________________________________________
2. Blood ________________________________________________________
3. Stool _________________________________________________________
4. T.B Test ______________________________________________________
5. Syphilis test ___________________________________________________
6. Urine examination ______________________________________________
7. Eye test ______________________________________________________
8. Chest test _____________________________________________________
9. Ears test ______________________________________________________
10. Spleen ______________________________________________________
11. Abdomen ____________________________________________________
12. Pregnancy (for girls only)________________________________________

**Any additional information:**

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

I certify that the above pupil is suitable/ unsuitable for taking secondary school studies. If unsuitable please give reasons:

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

________________________ ____________________ ________________________

Name of M.O Signature Date

Official stamp:

**<u>HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI</u>**

**<u>MCHINGA SEKONDARI</u>**

**<u>FOMU Na. 2: MAHITAJI MUHIMU YA SHULE</u>**

**1. <u>SARE:</u>**

**A.*Wavulana:***

- Suruali mbili rangi ya damu ya mzee kitambaa kizito cha suti. Suruali lazima ifunike visigino vya viatu na isiwe modo. **Mzazi simamia kwa umakini suala hili ili kuepusha usumbufu wa mtoto kurudishwa.**
- Mashati mawili meupe mikono mifupi ya kitambaa cha tetroni.
- Tai rangi ya damu ya mzee.
- Viatu vyeusi vya ngozi.
- Soksi nyeupe jozi mbili.
- Mkanda mweusi wa ngozi.
- Traki na t-shirt (jezi) rangi nyeupe pamoja na raba kwa ajili ya michezo.

**B.*Wasichana:***

- Sketi mbili ndefu kuvuka magoti za rinda za kupanga zenye rangi ya damu ya mzee, kitambaa kizito cha suti. **Mzazi simamia hili kwani ni marufuku kuvaa sketi fupi.**
- Masharti mawili meupe mikono mirefu (kama mtoto atavaa hijab) au mikono mifupi kama hatovaa hijab. Kitambaa ni tetroni na shati liwe na kola shingoni.
- Hijab nyeupe sana (kwa wanaohitaji kuvaa) ya kujihifadhi lakini isiwe kibwaya.
- Viatu vyeusi vya ngozi na visiwe na visigino virefu.
- Soksi nyeupe jozi mbili.
- Traki na t-shirt (jezi) rangi nyeupe pamoja na raba kwa ajili ya michezo.

**NB:** Kushiriki michezo kwa mwanafunzi hapa shule ni hitaji la lazima kiafya na kiakili hivyo vifaa hivyo ni muhimu mtoto kuwa navyo!

## 2. <u>MAHITAJI MUHIMU YA SHULE NA MWANAFUNZI</u>.

Kwasababu za usajili usafi binafsi wa mwanafunzi na mazingira ya kujifunzia ili uchukuaji wake wa masomo uwe mzuri zaidi, mwanafunzi anapaswa kuwa na vifaa vifuatavyo:

- Fagio moja ya chelewa (kuti la mnazi), ukubwa wa mkono wake,
- Daftari za kutosha kwa kuanzia 10, kalamu za wino na risasi na mkebe (mathematical set) 1, daftari ndogo za mazoezi pamoja na mfuko (begi) wa kutunzia na
- Kamusi ya Kingereza-Kiswahili au Kiswahili-Kingereza.

*************************************

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

**MCHINGA SEKONDARI**

**FOMU Na. 3: SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya kusimamia elimu nchini na Ofisi ya Raisi – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Katika kipindi chote utakachokuwa hapa, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

a) Heshima kwa Walimu, Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na Jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni jambo la lazima;
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio jioni (preparation);
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kufanya hivyo; na
h) Kutunza mali za shule.

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:**

a) Wizi,
b) Uasherati na ushoga,
c) Ubakaji,
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
e) Kupiga au kupigana,
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma,
g) Kudharau bendera ya taifa,
h) Kuwa mjamzito/Kupata mimba,
i) Kuoa au kuolewa,
j) Kutoa mimba,
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu,
l) Kukataa adhabu kwa makusudi, na
m) Kuwa na simu ya mkononi.

**************************************************

**<u>HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI</u>**

**<u>MCHINGA SEKONDARI</u>**

**FOMU Na. 4: <u>HATI YA KUKIRI NA KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE</u>**

**<u>A. MWANAFUNZI</u>:**

Mimi ……………………………………………………….ninakubali kuchukua nafasi niliyopewa katika shule ya Sekondari ya Mchinga . Ninaahidi nitatii sheria zote, kanuni na maelekezo yote yaliyotolewa na yatakayotolewa na shule na kwamba nitajitahidi na kushirikiana na Wanajumuiya wa Mchinga Sekondari katika shughuli zote za MASOMO, KAZI na MICHEZO katika kipindi chote cha uanafunzi wangu. Na kwamba kwenda kinyume na kukiri huku ni kutoa nafasi kwa hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi yangu.

Jina la Mwanafunzi………………………………….….….Sahihi ……..……………..… Tarehe………………….

**B: <u>MZAZI/ MLEZI</u>**

Mimi…………………………………………………………….ambaye ni Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……………………………………….., nakubali mtoto wangu ajiunge na shule ya Sekondari Mchinga na kufuata taratibu zote zilizowekwa. Nakubali kuwa nitatoa mahitaji yote ya mwanafunzi yanayonihusu pamoja na kufuata maelekezo yaliyotolewa na yatakayotolewa na shule kama inavyostahili. Nafahamu kuwa Kutotekeleza majukumu hayo kutapelekea nichukuliwe hatua za kisheria.

Jina la Mzazi/Mlezi:……………………..……..…Kazi…………………Kitongoji………………….Kijiji …………………………..Kata ………………………Uhusiano na mtoto……………………

Anuani ……………..........Sahihi………………… Tarehe………………Simu………………..

**C. <u>TAARIFA ZINGINE ZA MTOTO:</u>**

<u>i) **Mzazi/Mlezi mwingine**;</u>

Jina………………………………….Kazi……….…Uhusiano…………Kijiji……………….. Simu………………….

ii) **Malezi**

Je, mtoto ni yatima? Ndiyo/Hapana (kata isiyohusika). Kama ni yatima, amefiwa na baba/mama/wazazi wote (kata isiyohusika).

iii**) Afya**; je, mtoto ana ulemavu au ugonjwa wowote wa kudumu? Taja

Ulemavu…………………………………………………………………………………......

Ugonjwa wa kudumu…………………………………………………………………………….

iv) **Umri**: Tarehe na mwaka wa kuzaliwa mtoto……………………. Miaka ………

v) **Uongozi wa Mtaa/Kitongoji**

Jina la Mwenyekiti wa Mtaa/Kitongoji…………………..……….……..Simu…………………

Muhuri …………………